

**Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu EBT ya Utunzaji Mtoto
kutokana na Janga (P-EBT)
na P-EBT ya Utunzaji Mtoto ya Msimu wa Kiangazi (** Mpya)
Mwaka wa Masomo 2021-2022 (Tarehe 5 Agosti 2022)**

Swali la 1: Msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto ni nini?

Jibu: Ni msaada wa vyakula wa muda ulioidhinishwa na serikali ya shirikisho ili kusaidia kaya zilizo na watoto chini ya miaka 6 wakati wa janga la COVID-19.

Swali la 2: Nani anastahiki misaada ya P-EBT ya Utunzaji Mtoto?

Jibu: Kaya za Vermont zinazopokea msaada wa 3SquaresVT zilizo na watoto walio chini ya umri wa miaka sita. Misaada ya P-EBT ya utunzaji mtoto itatolewa kila mwezi kuanzia Septemba 2021 hadi Juni 2022 kwa kaya zinazostahiki.

Swali la 3: Je, msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto ni kiasi gani?

Jibu: Msaada wa P-EBT wa utunzaji mtoto ni \$32.31 kwa kila mtoto kwa Septemba 2021 hadi Januari 2022. Kiwango kwa Februari hadi Juni 2022 ni \$33.55 kwa kila mtoto kwa mwezi.

Swali la 4: Je, msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto katika Msimu wa Kiangazi ni kiasi gani?

Jibu: Jumla ya msaada kwa P-EBT ya utunzaji mtoto ya msimu wa kiangazi ni \$391 kwa kila mtoto. Tofauti na msaada wa kawaida wa Utunzaji Mtoto wa kila mwezi, msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto wa Msimu wa Kiangazi ni msaada wa kiasi kinachotolewa sawia kwa wote cha mara moja tu. ambao unahusika kwa miezi yote ya msimu wa kiangazi ya Julai na Agosti.

Swali la 5: Je, misaada ya P-EBT ya Utunzaji Mtoto itatolewa lini?

Jibu: Duru ya kwanza ya misaada (kwa Septemba 2021 hadi Januari 2022) itatolewa mwanzoni mwa Juni 2022. Watoto wanaostahiki msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto watapokea malipo ya kwanza kwa miezi ya msaada ya Septemba hadi Januari kwa kila mwezi ambao kaya hiyo ilipokea misaada ya 3SquaresVT.

Misaada kwa Februari hadi Juni 2022 itatolewa mnamo Septemba.

Malipo kwa msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto yatafanyika mnamo Septemba kwa kaya zinazostahiki 3SquaresVT mnamo Julai. Kwa kaya zenye ustahiki wa msaada wa 3SquaresVT kuanzia Agosti, msaada wa P-EBT wa Utunzaji Mtoto utalipwa mnamo Oktoba. Tarehe hizi zinaweza kubadilika, tafadhali endelea kutembelea tovuti hii kwa Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara yaliyosasisiwa.

Swali la 6. Ninawezaje kujua iwapo kaya yangu inakidhi mahitaji?

Jibu: Kitengo cha Huduma za Kiuchumi (ESD) kitaamua kama mtoto wako anastahiki, kulingana na vigezo vya hapo juu. Ikiwa unastahiki, utapata barua kutoka ESD inayoelezea jinsi gani na lini utapata msaada.

Swali la 7: Ikiwa tunastahiki, je, tutapokea vipi misaada hii?

Jibu: Misaada ya P-EBT ya Utunzaji Mtoto hutolewa kwenye kadi ya EBT ambayo ilitolewa kwa kaya yako kwa msaada wako wa 3SquaresVT.

Swali la 8: Malezi ya mtoto wangu yamegawanyika baina ya kaya mbili. Nani atapata msaada?

Jibu: Msaada huo utatumwa na ESD kwa mtu mzima ambaye ameorodheshwa kama Mkuu wa Kaya katika mpango wa msaada wa 3SquaresVT.

Swali la 9: Ninaweza kununua nini kutumia msaada huu?

Jibu: Tazama [orodha ya vyakula vinavyostahiki](#) kwenye tovuti ya USDA.

Swali la 10: Ninaweza kutumia wapi kadi yangu ya EBT?

Jibu: Unaweza kuitumia kununua vyakula katika eneo lolote ambalo linapokea 3SquaresVT. Hii ni pamoja na maduka ya vyakula, maduka makubwa, maduka ya karibu, na masoko mengi ya wakulima katika Vermont. Pata maelezo zaidi kwenye [ukurasa wa EBT wa tovuti ya DCF](#).

Swali la 11: Sina watoto walio katika huduma ya utunzaji mtoto. Je, naweza kupata msaada huu?

Jibu: Ndiyo. Watoto wote walio chini ya umri wa miaka sita na ambao wanapokea msaada wa 3SquaresVT wanastahiki.

Swali la 12: Nina watoto wengine wakubwa zaidi ya miaka sita. Je, wanastahiki msaada wa P-EBT wa utunzaji mtoto?

Jibu: Hapana. Msaada unapatikana tu kwa watoto ambao wanapokea msaada wa 3SquaresVT na walio chini ya umri wa miaka sita. Tafadhali angalia Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara ya P-EBT kwa maelezo zaidi kuhusu misaada inayopatikana kwa watoto wenye umri wa kwenda shule.

Swali la 13: Je, itakuwaje iwapo sitaki msaada huu?

Jibu: Ushiriki ni kwa hiari. Ikiwa utachagua kutoshiriki, usitumie misaada ya ziada inayotolewa kwenye kadi yako ya EBT ya 3SquaresVT.

Swali la 14: Je, msaada wa P-EBT una tarehe ya mwisho ya matumizi usipotumiwa?

Jibu: Ndiyo. Misaada ya P-EBT itakoma ikiwa kadi haitatumika ndani ya siku 274.

Swali la 15: Nina maswali zaidi. Ninaweza kupata maelezo zaidi wapi?

Jibu: Tembelea <https://dcf.vermont.gov/esd/covid19/P-EBT> au piga simu 1-800-479-6151 chagua 7 kwa maelezo zaidi.